Ukweli wa Mambo

Toleo la Kwanza la Kauli ya nguvu ya Hoja | Ndugu **Mwandawiro Mghanga** | May – Juni 2007

Msesighe Mwavalenyi Mkimbirie Mwaisakenyi

Kufungamana na jukumu la kuwa mbunge wenu, kwangu huu si wakati wa kampeni kwani kipindi cha bunge la tisa kingaliko. Ni wakati wa kuendelea kushirikiana nanyi nyote kuchapa kazi mliyonipa na ambayo naipenda na naiheshimu sana, pamoja na magumu na majaribu yake yote. Huu ndiyo ukweli wa mambo.

Shukrani kwenu watu wetu wa Wundanyi, bado mimi ni mbunge wenu. Na nitaendelea kuwatumikia kwa uwezo wangu wote hadi bunge litakapovunjwa, panapo majaliwa ya Mwenyezi Mungu. Basi wakati huo ndipo nitarudi kwenu tena kuwaomba kura zenu ili niendelee kuwatumikia na kuwawakilisha.

Hapo nitawakumbusha kuwa nitakuwa nimewatumikia kwa miaka mitano tu, kipindi cha kuanza kutekeleza mambo. Sijachoka nanyi na nina hakika hamjachoka nami. Hivyo basi, sina wasiwasi, nitakitetea kiti cha Wundanyi ipasavyo, bali wakati ukifika. Kwa sasa bado mimi ni mbunge wenu, tuendelee kushirikiana bega kwa bega kusukuma gurudumu la maendeleo Wundanyi. Kufungamana na jukumu la kuwa mbunge wenu, kwangu huu si wakati wa kampeni kwani kipindi cha bunge la tisa kingaliko. Ni wakati wa kuendelea kushirikiana nanyi nyote kuchapa kazi mliyonipa na ambayo naipenda na naiheshimu sana, pamoja na magumu na majaribu yake yote. Huu ndiyo ukweli wa mambo.

Ni ukweli pia kwamba kampeni za wapinzani zimechacha sana kila pahali Wundanyi, kama sehemu nyingine nchini. Ni wengi wapinzani Wundanyi, wengi sana. Wanazunguka kila pahali, usiku na mchana siku nenda rudi. Mara wakinishambulia, mara wakidai ati wao ni mashujaa, mara wakiniita Mungiki, mara wakiahidi hili au lile, mara wakimwaga pesa huku na kule, almradi wanataka kura zenu! Ni kutokana na ukweli huu ambapo kwa jina la uhuru na demokrasi, na nikiwa mtumishi wenu mwaminifu, sina budi kueleza yafuatayo maana kuna wengine ambao wanafanya kampeni za kueneza uongo, chuki na kutia wasiwasi miongoni mwa wananchi:

Kwanza, kiti cha ubunge cha Wundanyi ni kiti cha watu wa Wundanyi na Wakenya kwa ujumla. Hivyo, kila mwananchi wa Wundanyi na Kenya ana haki ya kukipigania. Ndiyo sababu sina chuki na yoyote yule anaenipinga kwani daima napigania haki za binadamu siyo tu nchini bali ulimwenguni kote. Na kushiriki kwa kampeni za kutaka kuchaguliwa kuwa kiongozi ni haki ya kidemokrasi ambayo ni haki ya binadamu pia katika dunia ya sasa. Nimeitetea na nitaendelea kuitetea. Aidha, sina hofu wala wasiwasi kwa kuwepo kwa wapinzani chungu nzima. Mimi ni mwanamapinduzi tena mkereketwa wa demokrasi ya mfumo wa vyama vingi. Na

Nikisukumwa Jela ya Kamiti Maximum, 1985.

Wakati wapinzani wangu wakuu walikuwa wakiutetea mfumo wa udikteta na wa kuvunja haki za binadamu sisi tulikuwa upande wa wananchi tukipigania ukombozi kwa dhiki na kusaga meno.

Tukumbuke sisi ni nani, tumetoka wapi na tunafun

tuwache watu wajitokeze, waseme yao, wasikilizwe, waonekane wazi, hatimaye wapiga kura wenyewe wataamua anaetosha ni nani. Kwa nini niogope upinzani na nilikuwa katika msitari wa mbele wa kupigania demokrasi ya mfumo wa vyama vingi? Wakati wapinzani wangu wakuu walikuwa wakiutetea mfumo wa udikteta na wa kuvunja haki za binadamu sisi tulikuwa upande wa wananchi tukipigania ukombozi kwa dhiki na kusaga meno. Wakati wao walikuwa wakizawadiwa na mfumo wa udhalimu na ufisadi kwa vyeo, pesa, majumba, mashamba na maploti, sisi tulilazimika kuishi gerezani na uhamishoni tuking'ang'ana na tabu za kila aina. Wao waliamua kuwa waoga wa kujali masilahi yao tu, sisi tuliamua kujitoa mhanga kupigania uhuru wa nchi yetu. Na leo haizuru tumepiga hatua kadhaa mbele za uhuru, demokrasi na haki za binadamu nchini. Bali ukombozi haubagui, ni wa kila mtu, hata yule aliekuwa akiupinga ukombozi wenyewe. Hivyo, nitaendelea kutetea haki ya kila mtu – mkiwemo wapinzani wangu – wa kushiriki katika siasa za Wundanyi na Kenya. Isipokuwa tu kama kiongozi nina jukumu la kuwakumbusha watu wa Wundanyi, demokrasi inahitaji kutunzwa, kulewa na kulindwa. Nina haki ya kusema kwamba naona bado ni mapema mno kuanza kufikiri tunaweza kuiwachia demokrasi kutunzwa, kulewa na kulindwa na maadui wake wa jana tu! Lazima tuwe na sababu za kufanya mabadiliko, tujihadhari watu wa Wundanyi tusishawishiwe kufanya mabadiliko ya kuturudisha nyuma tuliko toka. Tunaenda mbele, lazima tuendelee kwenda mbele daima. Kwani huu ni ukweli mtupu wa mambo.

Pili, kuitunza, kuilea na kuilinda demokrasi ni kufanya siasa kwa amani, bila chuki.

Mimi sikuchukii na unadai kiti ninachokishikilia kwa sasa, mbona wewe unanichukia kana kwamba mimi ni adui wako mkubwa? Mbona siasa zako ni za matusi na masengenyo na za kuombeana mabaya? Wenzangu, demokrasi si vurugu, demokrasi ni kutafuta uongozi bora. Tushiriki siasa kwa amani, tukiheshimu kila mtu hata kama hatukubaliani nae. Ya nini tufanye njama za kuharibu majina ya wengine tukidhani tunafanya siasa? Tena tusisahau kuwa tu Waafrika wenye mila na tamaduni, tuheshimu wake, wakwe na mashemeji zetu, ukoo: *Ihehe ja wulongozi jisedibonye kuchambia wupe ghodu bila waya*! Tukumbuke sisi ni nani, tumetoka wapi na tunafundisha nini vizazi vya leo na vijavyo. Kwa sababu ukiwa kiongozi utawakilisha kila mtu, aliekupigia kura na ambae hakukupigia, mfuasi wako na mpinzani wako, ndipo kunakuwa na maendeleo na demokrasi inaonekana. Kwa sasa nawakilisha kila mtu Wundanyi, hata nyie wapinzani wangu, basi siwezi kudharau au kuchukia yoyote. Na huu pia ni ukweli wa mambo.

Tatu, hebu tuseme ukweli na tujitenge na uongo.

Nimesema kuwa mimi bado ni mbunge wa Wundanyi na wakati ukifika nitajitokeza kimadhubuti kukitetea kiti cha ubunge cha Wundanyi ninachokishikilia sasa huku nikiwashukuru watu wa Wundanyi. Mbona wewe unadai kura kwa kudanganya watu ati tulikubaliana nitakuachia kiti hiki baada ya miaka mitano? Nikuachie kwani kiti cha watu wa Wundanyi na Wakenya ni mali yangu? Isitoshe, hatujawahi hata siku moja kuwa upande mmoja wa kisiasa na

Tushiriki siasa tukicheka kwa amani na furaha.

disha nini vizazi vya leo na vijavyo

"Sisi tutatoa kile tulicho nacho", tukichanga Marumange

wulongozi jisedibonye

Ihehe ja wulongozi jisedibonye kuchambia wupe ghodu bila waya!

tena u mpinzani wangu, iweje tushirikiane kisiasa wakati huu? Ikiwa mara nyingi uliwaambia watu wa Wundanyi kuwa hutaingia siasa hata siku moja na sasa umeamua kufanya hivyo, si hayo ni yako na Mungu wako na wapiga kura wa Wundanyi! Yananihusu nini mie? Maji umeyavulia nguo, hebu vumilia uyaoge! Na chunga usitoke nje uchi ati sababu unayaoga! Si mimi nimesema kila mtu ana haki ya kugombea kiti chochote cha uongozi? Bali huna haki ya kufikiria au kudanganya kuwa nitakuwachia kiti? Ukiwa nani? Karibu tukigombanie. Narudia, wakati ukifika nitawaeleza watu wa Wundanyi kuwa nina sababu nyingi za kutosha za kuwaomba mara nyingine wanirudishe tena bungeni niendelee kuwawakilisha. Na huu vilevile ni ukweli mwingine wa mambo.

Nne, siasa za kidemokrasi si za kuwagawanya watu wa Wundanyi au Kenya bali ni kwa ajili ya kuwaunganisha ili kuwapa fursa ya kusulihisha mambo yao ya kisiasa, kiuchumi, kijamii na kiutamaduni kwa mpango na kwa amani. Demokrasi inafungua uwanja wa kumaliza tofauti zetu bila kugombana au kupanda mbegu za vita na uhasama miongoni mwetu. Hivyo basi, kwa nini unaandika na kusambaza maandishi ya kuharibu majina ya watu huku ukidanganya ati ni kumbukumbu za mkutano wa siri wa kisiasa wa watu mashuhuri Wundanyi? Si huko ni kupanda mbegu za uhasama tena za kupinga demokrasi? Hata kama ingelikuwa ni kweli watu walikutana kupanga siasa zao hata za kunipinga, walikosa nini na ni haki yao ya kidemokrasi? Watapangaje siasa zao bila kufanya njama? Wewe hufanyi njama za siri za kisiasa na wafuasi wako, tena za kunipinga? Nikiwa mbunge wa nguvu ya hoja sikubali wala sintakubali kuletewa siasa duni za udaku, fitina na masengenyo. Mimi ni mbunge wa Wundanyi sio mfalme wa kutawala watu wa Wundanyi. Na huu pia ni ukweli wa mambo.

Tano, kwa vile umezaliwa au unaishi Mgange, Werugha, Wumingu, Mbale au Kwaweni Kese au Mwafunja si sababu ya kutosha ya kukufanya utegemee kupigiwa kura na watu wa Mgange, Werugha, Wumingu, Mbale, Kwawenikese au Mwafunja. Nani huchagua anapozaliwa, au ukoo wake au kabila lake au jinsia yake? Tunataka siasa za nguvu ya hoja sio za kuwagawanya watu wa Wundanyi kiukoo au kisehemu. Tunahitaji Kenya moja bali inayotawalwa kimajimbo lakini siyo kiukoo na kiukabila. Isitoshe, tunaelekea kuwa na Shirikisho la Afrika Mashariki, basi mbona wewe unaendelea kuwarudisha watu nyuma kwa kuhubiri siasa duni za Kwaweni Kese na Mwafunja, Mgange Dawida na Mgambonyi, n.k. Basi hiyo si siasa ya kimaendeleo. Siasa ya kimaendeleo ni siasa ya kuleta hoja. Hoja ya kumulika barabara sahihi ya ukombozi wa jamii, ya kuelekeza watu kujikomboa kutoka kwa umaskini na udikteta. Hoja ya kuwapa watu matumaini ya ukweli ya kujenga ulimwengu mpya wa maisha bora ya kuhakikisha kila mtu anashiriki katika kufaidi kutokana na rasilimali za nchi yetu ili aishi maisha ya kiutu. Tufanye siasa za kujenga watu, kuinua watu kifikra na kiutu wala siyo za kutumia watu. Fanya watu wajue haki zao, kama ninavyoendelea kufanya kila siku, siyo wabaki daima wa kuambiwa na kusifu na kuabudu binadamu. Huu tena ni ukweli wa mambo.

Sita, usitumie pesa kama fimbo. Kama una pesa tupe, tule, tutumie kuharakisha maendeleo. Ukichanga, changa kwa ukarimu na tutakushukuru. Sisi tutatoa kile tulicho nacho, nacho pia kitabarikiwa vilevile. Nitatenda bila kujisifu. Bali kushawishi watu kwa shilingi hamusini na kilo ya sukari, kutegemea watu watakuchagua kwa ajili tu ya hela unazomwaga kwa kiburi na kiherehere kila pahali, kuwahonga, huko ni kuwadharau na kuwadunisha watu. Na kama hujui, watu hasa wa Wundanyi, ni werevu sana kuliko unavyofikiria.

Nawashukuru watu wetu sana kwa sababu hampigii mtu kura kwa sababu amemhonga na pesa. Mmeonyesha kwamba mnapigia ukweli wa hoja, siasa za kimaendeleo za mwanga wa matumaini. Mnaelewa tulikotoka, tulipo sasa na dalili za tunapoendelea pia mnaziona. Ndiyo kwa maana nina imani kuwa mnachuja na kuchekecha yote yanayopangwa na kusemwa na wapinzani wangu. Na wakati utakapofika mtaamua kwenda mbele wala siyo kubahatisha na watu wapya wakati tayari mna nguvu ya hoja. Na huu pia ni ukweli mwingine wa mambo.

Saba, asanteni watu wa Wundanyi na Taita - Taveta kwa ujumla kwa kuitikia mwito na kujitokeza kwa wingi kwa maandamano ya kudai haki Taita – Taveta, Wundanyi. Si kitu, wapinzani wangu na wakiwa baadhi ya madiwani wa Baraza la Taita – Taveta walikataa kushiriki hata wakanilaani na kukashifu mapambano yenyewe magazetini. Mimi sitarudi nyuma katika kutetea haki za watu wetu, ninafahamu majukumu yangu kama mbunge. Vilevile, najua kuwa maandamano ya amani ni haki ya kikatiba ya raia. Lazima tutetee ardhi na rasilimali za Taita bungeni, ikibidi kwa maandamano na kwa kila hali. Kama mbunge nina wajibu wa kuongoza mapambano dhidi ya ufisadi na njama zozote zile za kudanganya, kupuuza na kudhulumu watu wa Wundanyi. Mapambano ya haki ni halali hata mbele ya Mwenyezi Mungu. Na huu ni ukweli wa mambo vilevile.

Nane, maadui zangu serikalini na vibaraka wao wanaopambania kiti cha ubunge cha Wundanyi wanatumia kila njia kuharibu jina langu. Wako tayari hata nifungwe au hata waniue ili nisiwe mbunge wa Wundanyi leo na kesho. Sababu hawawezi kunisingizia ufisadi sasa wananihusisha na Mungiki. Mimi nawaambia hivi: sijawahi kuwa mwanachama wa Mungiki wala hiyo Munguki haijawahi kuwa au kuonekana Wundanyi au Taita – Taveta nikiwa mbunge. Daima ninahubiri amani na demokrasi huku nikitetea haki za watu wa Wundanyi na Wakenya bila woga wala hofu. Si ajabu kwamba nikihesabiwa mojapo wa wabunge wanaochangia zaidi bungeni na ambae niko pamoja na wananchi wa Taita – Taveta kila mara katika harakati za kudai haki zao, nimepangiwa njama - ambazo hazitafua dafu - za kuniharibia jina kwa kila hali ati ili watu wachoke nami. Wala si bahati kuwa nimeanza kupigwa vita zaidi huku nikiwa na Raila Odinga sehemu ya Kisii nikimsindikiza katika kampeni zake za urais. Serikali inashindwa kulinda usalama wa wananchi hasa wa Mkoa wa Kati, Nairobi, Mlima Elgon na kote nchini halafu wanamsingizia Mwandawiro! Mimi si waziri wa usalama! Tena ni bora wajue mapema ukweli kwamba propaganda zao chafu za kuniharibia jina hazitanifanya ninyamaze bungeni wala hazitanifanya nikose kudai utawala bora zaidi nchini. Kwani kweli haihofu tisho wala nguvu za majeshi na uongo una mwisho wakati ukweli hudumu milele. Tena kweli itashinda kesho kama leo haishindi. Na huu ni ukweli wa mambo kabisa.

Tunaenda mbele, lazima tuendelee kwenda mbele daima, Wundanyi.

Mwisho, kwa wale ambao hawana kura, kura zitaandikishwa tena na kwa mara ya mwisho kuanzia mwezi huu wa Juni kwa muda wa mwezi mmoja. Natarajia kuwa watu watajiandikisha kama wapiga kura kwa wingi kote Wundanyi. Kwani katika mfumo wa demokrasi, kura ni silaha ya nguvu yenye uwezo wa kuboresha maisha. Kumbuka kura yako ndiyo itakayosaidia kuamua ukweli wa mambo. Jiandikishe na wakati ukifika ujitokeze uipige kura yako, kwangu. Ninaihitaji, tunaihitaji sote tunaotaka kwenda mbele daima.

Ukweli wa Mambo tutaendelea kutetea na kueneza siasa zenye sera, za kujenga na kukuza: za amani, ukweli, haki, demokrasi, maendeleo, uhuru, ushujaa na ukombozi – siasa za nguvu ya hoja. Huu ni mwanzo tu.

KAENYI PANANA NA SERE YA MLUNGU KARI KOSE!!!

CONTACT: Telephone: 254 – 20 – 2848540 Ext. 32540 Email: mwandawiro2002@yahoo.com